

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

MKURUGENZI WA JIJI LA MWANZA
Simu: +255 28 2501375
Nukushi: +255 28 2500785
Barua pepe: cd@mwanzacc.go.tz
Tovuti: www.mwanzacc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI,
JIJI LA MWANZA
S.L.P 1333,
MWANZA

9 Februari, 2017

TAARIFA KWA UMMA

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Bi. Mary Onesmo Tesha amefanya majumuisho ya ziara za kikazi alizozifanya katika kata 18 za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Katika majumuisho hayo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ametoa maagizo yafuatayo:-

Agizo la kwanza, Watumishi wote wanatakiwa kuishi karibu na vituo vyao vya kazi. Vilevile Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya amewataka Maafisa Watendaji wa kata kushirikiana na Wakuu wa shule za Msingi na Sekondari kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye umri wa kujiandikisha kwenda shule na waliofaulu kwenda kidato cha kwanza wanaandikishwa.

Kwa Kuongezea Mhe Mkuu Wilaya amepiga Marufuku uuzaji wapombe kabla ya saa 10.00 Jioni na Vileo kuuzwa katika maduka ya kuuza bidhaa za majumbani, **“nimebaini katika ziara nilizozifanya katika kata kuwa kuna watu wanalewa wakati wa kazi hivyo ni marufuku na Afisa mtendaji yeyote ambaye kwenye eneo lake atakutwa mtu analewa wakati wa kazi ama maduka ya kawaida yanauza pombe hatachukuliwa hatua kali za kisheria”**

[Type here]

Mwisho, Mhe Mkuu wa Wilaya amewapongeza na kuwashukuru Wah.Madiwani pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi ya Jiji la Mwanza Kwa Ushirikiano mzuri waliotoa Kwa Muda wote wa Ziara ya Mhe Mkuu wa Wilaya Ya Nyamagana.

Martin Sawema

Afisa Habari ,Halmashauri ya Jiji la Mwanza

9 Februari 2017.

[Type here]